Received 03-12-2024

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**


*Simu: +255 26 2605546*
*Nukushi: +255 26 2605546*
*Barua pepe: acl.dar es salaam@ardhi.go.tz*
*Web:www.ardhi.go.tz*

Ofisi ya Kamishna wa Ardhi
Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam
1 Mtaa wa Ardhi
S. L. P. 9132,
**11477 DAR ES SALAAM.**


Tafadhali unapojibu taja:
**Kumb. Na. LD/388863/16**

**20/11/2024**

Mkurugenzi Mtendaji,
Asialilac Apparel (Tanzania) Company Limited,
S. L. P 1212,
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KUTANGAZA NA KUMILIKISHA VIWANJA NA 1376, 1377 & 1378 KITALU "B" ENEO LA UBUNGO SOUTH, MANISPAA YA UBUNGO KWA AJILI YA UWEKEZAJI**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Tulipokea maombi ya kutangaza na kumilikisha viwanja tajwa hapo juu kwa ajili ya Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa maslahi ya Kampuni ya **ASIALILAC APPAREL (TANZANIA) COMPANY LIMITED** yenye cheti cha uwekezaji **Na. 202361259.**

3. Kwa mujibu wa nyaraka zilizoambatishwa na maombi haya, mlipata viwanja tajwa kwa njia ya mauziano kutoka kwa wamiliki wa awali na baadhi ya wauzaji walishakuwa na hati miliki na taratibu za uhamisho wa miliki zimekamilishwa.

4. Kumbu kumbu zilizopo zinaonesha viwanja husika vimepangwa kwa matumizi ya Makazi. lakini taarifa za cheti cha uwekezaji, zinaonesha mradi tarajiwa ni Ujenzi wa nyumba za makazi zaidi ya familia moja **(Apartments).** Hivyo, tunaomba kutuwasilishia taarifa kuhusiana na aina ya nyumba **(Apartments)** zinazotarajiwa kujengwa katika viwanja hivi mkianisha idadi ya sakafu.

5. Taarifa hiyo ni muhimu ili kutuwezesha kuwashauri kuhusiana na Mpango wa uendelezaji wa maeneo hayo.

Tunategemea ushirikiano wenu.

Bishanga, T.H
**K.n.y: KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI**
**MKOA WA DAR ES SALAAM**